# NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO

## "KABUMBU AFRIKA- NI ZAIDI YA MCHEZO!"

## EPISODE FIVE: "Maadui uwanjani, maswahiba hatimaye"

**MWANDISHI : Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Thelma Mwadzaya**

**Orodha ya washiriki/ KIPINDI CHA TANO**

- Msimulizi

**SCENE ONE: SOCCER CLINIC AT CITY STADIUM**

- Chedede ( mume,14 )
- Safina ( mke,13 )
- Jonathan ( mume, 15 )
- Metogba ( mume, 28 )
- Komora ( mume, 14 )
- Sauti mchanganyiko za wasichana na wavulana (13+)

**SCENE TWO: THE PHONE CALL**

- Hon. Makemba. ( mume, 55 )
- Aunt Lily ( mke, 33 )

**SCENE THREE: THE MATCH BETWEEN TWO FRIENDS**

- Chedede ( mume,14 )
- Safina ( mke, 13 )
- Jonathan ( mume, 15 )
- Metogba ( mume, 28 )
- Komora ( mume, 14 )
- Sauti mchanganyiko za wasichana na wavulana (13+)
- Wakasa ( mwenyekiti wa shirikisho la soka, mume, 54 )

**SCENE FOUR: MAKEMBA AND SON RIDING HOME**

- Mhe. Makemba. ( mume, 55 )
- Jonathan ( mume, 15 )

**SCENE FIVE: AT AUNT LILY'S**

- Chedede ( mume, 14 )
- Safina ( mke, 13 )
- Aunt Lily ( mke, 33 )

**INTRO:**

1. **NARRATOR:** Hamjamboni na karibuni tena katika kipindi cha Noa Bongo,Jenga Maisha yako tukiendelea kuipepeta hadithi yetu ya soka ” **Kabumbu afrika- Ni zaidi ya mchezo!”.**Kama wahenga walivyonena "Kikulacho ki nguoni mwako" yaani, ”Aghalabu,anayekudhuru ni yule anayekujua vizuri!”.Somo hilo ndilo lililokuwa likimsubiri Chedede, kijana mdogo wa mtaani.Jee Safina naye ameamua vipi kuhusu kujiunga na kliniki ya mazoezi ya soka?Shangazi yake ataupokea vipi uamuzi huo?Unalikumbuka lile dirisha lililovunjwa?Jee,Metogba ana mpango wowote wa kuwachukua vijana wanaotumiwa na waasi mwituni wajiunge na kliniki yake ya soka?Timu hoyo itaendelea kuwa kitu kimoja au itasambaratika?Baki nasi uyajue yote hayo katika makala hii ya**" Maadui uwanjani:Maswahiba hatimaye ".T**unaanza na Chedede na Safina wanaoelekea kwenye uwanja wa michezo.

**SCENE ONE:SOCCER CLINIC AT THE CITY STADIUM**

2. **SFX: FOOTBALL PLAYING SOUNDS COMING NEARER**

3. **CHEDEDE:** Safina, sidhani kama hili lililkuwa wazo zuri.

4. **SAFINA:** Kwanini?,hakuna ubaya kuja kutazama. Usiwe na wasiwasi, haja yetu ni kumuona Metogba na kuwajua hao wachezaji, halafu tuondoke. Kwanza ndio wale nawaona wako katikati ya uwanja.

5. **METOGBA:** Ala,kuna wengine bado wanakuja . Inaonekana ipo shida kubwa mno ya watu kufika kuchelewa **.**

6. **KOMORA: (shocked)** Masalaale! Urafiki wangu na Dede umekwisha!

7. **CHEDEDE: (shocked)** Haiwezekani! Yule si Komora? Msaliti, unawezaje kufanya hivyo? **(raving angry)** nitakufunza adabu!

8. **SFX: SCUFFLES, FISTS AND FIGHT ON THEGROUND/MURMURS OF BOYS AND GIRLS**

9. **METOGBA: (Shouts )** Nyinyi! Hebu, acheni vita! acheni huu wazimu! Unafikiri wewe ni nani? Una haki gani ya kuja hapa kuanzisha mapigano na mmoja wa wachezaji wangu?

10. **CHEDEDE: (fuming)** Ni... ni... samahani sana lakini... **(words fail him)**

11. **SAFINA:** Wacha nikueleze, Metogba, Komora na Dede ni marafiki. Huyu Dede, alimwelezea Komora kuhusu hii kliniki baada ya kuzisikia taarifa hizo kwenye runinga. Lakini Komora akamvunja moyo na

kumuambia kuwa, haina haja ya kupoteza muda wake kuja huku, kwa sababu timu ilikuwa tayari imeshatimia. Kwa hivyo Dede akaamua hatokuja kujisajili. Lakini kwa bahati tumekuja hapa, kisha tunamwona nani? Komora!

12. **METOGBA:** Komora, haya asemayo huyu ni kweli?

13. **KOMORA: (embarrased)** Ndio, mkufunzi... nilijuwa atanipa ushindani akiwa katika timu. Sasa ningefanyaje? Lazima mtu ajitetee kivyake huku nje, ujanja ni lazima ili uweze kufanikiwa. Kila mtu nguvuze.

14. **CHEDEDE:** Wawezaje kusema hivyo? Nilikuamini kwa sababu ni rafiki yangu mkubwa. Nilikuchukulia kama kaka yangu… kama pacha mwenzangu.

15. **METOGBA:** Sawa, hakuna haja ya kupigana kama wanyama. Tuyamalize haya sasa hivi. Komora, ichague timu yako. Dede, pia fanya hilo kisha tutakuwa na mchuano kati ya timu hizi mbili. Mimi nitakuwa mpiga kipenga. Dakika kumi na tano pekee. Ni sawa, Dede?

16. **CHEDEDE:** Sawa, sina tatizo. Lakini nina ombi moja. Kwamba huyu rafiki yangu Safina acheze upande wangu, na angalau wasichana wengine wawili na mvulana yeyote mmoja.

17. **JONATHAN:** Nitakuwa kwenye timu yako.

18. **METOGBA:** Vyema! Jikusanyeni na kwenye timu zenu na muna dakika tano za kujiandaa. Mukisikia kipenga changu nataka Komora na

Dede munifuate nitakapokuwa. Tumeelewana?

19. **NARRATOR:** Ilikuwa dhahiri kuwa marafiki hao wa zamani hawakufurahiana, walipokua wakichagua wachezaji wao… Kwa upande mwengine, nje ya nyumban ya shangazi Lily kulikowa na gari la kifahari lilokuwa limeegeshwa. Madirisha ya gari hilo yalikuwa meusi na Mhe. Makemba alikuwa amekaa kwenye kiti cha nyuma akizungumza na simu yake ya mkononi.

**SCENE TWO: THE PHONE CALL**

20. **SFX: MOBILE PHONE NUMBER CALLING**

21. **SHANGAZI LILY: (through the phone)** Naam, haloo... Lily hapa. Nani mwenzangu?... Halo?... Haloo?

22. **MHE. MAKEMBA:** Lily? Salamu nyingi kwanza, najua ni muda mrefu...

23. **SHANGAZI LILY:** Nani mwenzangu? unanijuaje? Nani aliyekupa nambari yangu ya simu?

24. **MHE. MAKEMBA:** Ningependa tukutane. Niko garini nje ya nyumba yako….

25. **SHANGAZI LILY:** Hapana! Siko nyumbani kwa sasa. Isitoshe mpwa wangu amekuja kunitembela na yuko nyumbani saa hizi, kwa hivyo hatuwezi kukutana huko. Tafadhali nipigie wakati mwengine. Kwa heri.

26. **SFX: SHE HANGS UP**

27. **MHE. MAKEMBA:** Hallo?..Lily? Lily!. **(To driver)** Dereva, hebu twende zetu.

28. **SFX: CAR ENGINE STARTS, CAR DRIVES AWAY**

29. **NARRATOR**: Simu ya mhe. Makemba bila shaka ilikuwa ni ya utata. Alitaka kumuuliza nini shangazi Lily, ambaye alikuwa hamkumbuki? Mbali na hayo, shangazi Lily alielekea nyumbani upesi, hasa alipokumbuka kuwa kamuacha mpwa wake pekee. Hata hivyo hakujua kuwa Safina hakuwepo nyumbani… alikuwa kwenye uwanja wa michezo… wa jiji.. Huko uwanjani, mchuano kati ya timu ya Chedede na Komora ulikuwa tayari ushaanza.

**SCENE THREE: THE MATCH BETWEEN TWO FRIENDS**

30. **SFX: VOICES AS WHEN PEOPLE PLAY FOOTBALL**

31. **CHEDEDE:** ..Hapa, hapa..nipe pasi!

32. **SFX: BALL BEING KICKED...**

33. **CHEDEDE: (In agony)** Aaaauh!..

34. **SFX: WHISTLE BLOWS, FOOTBALL SOUNDS STOP**

35. **METOGBA: (Shouts**) Hiyo ni ngwala! Penalti kwa kikosi cha Chedede, Komora, hilo ni onyo la mwisho, ukicheza tena rafu nitakuonyesha kadi nyekundu.

36. **CHEDEDE: (Breathing heavily )** Safina, piga hiyo penalti.

37. **SAFINA: (Tired)** Mimi? Hapana! Kwa nini mimi? Wewe ndiye umecheza rafu.

38. **CHEDEDE:** Unaweza, nina imani. Hata mimi ulinifunga. Jikakamue.

39. **SAFINA:** Sawa... nitajaribu...

40. **METOGBA**: Zimesalia sekunde hamsini, mabao bado ni bila kwa bila. Chedede, mumeshaamua atakayeicharaza penalti hiyo?

41. **SAFINA:** Ni mimi.

42. **METOGBA:** Golikipa, uko sawa?

43. **SFX: WHISTLE IS BLOWN… BALL KICKED - HITS GOALPOST...**

44. **SAFINA/CHEDEDE/VOICES: (Disappointed)** Aaaaghgh!!!!!

45. **SFX: FINAL WHISTLE BLOWS THREE TIMES**

46. **METOGBA:** Kwisha! Mpira umekwisha! Njooni nyote mufanye mduara. Sikilizeni, dimba ni mchezo wa upendo, mpira wa kuimarisha urafiki na uhusiano wa kudumu miongoni mwa wachezaji, wakufunzi, mashabiki na hata wafadhili. Ndio, ni kweli huwa tunatofautiana, tunapapuana. Baadhi ya wakati wachezaji hupigana kama mlivyoshuhudia hii leo. Pindi mchuano ukikamilika, daima tunapeana mikono. Kwa hivyo nawataka nyinyi wawili mupeane mikono, Chedede na Komora. Naamini munaweza kufanya hilo.

**47. SFX:CHEERS AND APPLAUSE FROM OTHER PLAYERS.**

**48. METOGBA:** Haya tumekamilisha ya leo.Tuonane kesho saa mbili asubuhi. Dede, Komora na Safina, kidogo tuzungumze...

**49. SFX: SOUNDS OF PLAYERS WALKING AWAY AND CHATTERING, WHILE DIALOGUE CONTINUES.**

**50. CHEDEDE:** Metogba, samahani kwa yaliyotokea, ni vile nilishindwa kujizuia...

**51. METOGBA:** Hayo tuyasahauni. Kamwe sitaivumilia tabia ya namna hiyo katika siku zijazo. Swali ni nyinyi wawili muko tayari kujiunga na kliniki ya soka? Lazima nikiri kuwa Dede, una ujuzi mzuri wa kupepeta mpira, na Safina, lo! Uwezo wako ni wa hali ya juu kama mchezaji wa kulipwa!

**52. SAFINA: (Excited )** Mimi? Niko tayari kushiriki. Usinisahau!

**53. CHEDEDE:** Hata mimi.

**54. METOGBA:** Vizuri sana, kwa hivyo tuonane kesho. Bwana Wakasa! **(to Chedede na Safina)** Huyu ni bwana Wakasa, mwenyekiti wa shirikisho la soka. **(To Mr Wakasa)** Unaweza kutuandalia usafiri wa kurejea hotelini tafadhali?

**55. WAKASA:** Hakuna neno.Kuna jengine?

**56. METOGBA:** Ndio, tafadhali muite tena yule mwandishi wa habari

aliyenihoji awali Ili tuandae mkutano mwengine na waandishi wa habari.

**57. WAKASA:** Mkutano mwengine? Wa nini tena?

**58. NARRATOR**: Haswa! Mkutano mwengine wa nini? Metogba alikuwa na kipi chengine cha kuwaelezea wakaazi waTambarare safari hii? Kitabainika hivi punde. Safina na Chedede walifurahi sana baada ya kupewa nafasi ya kushiriki katika kliniki ya mazoezi ya soka. Baada ya mazoezi, Dede alimpeleka Safina kwenye duka la Shah Electronic, ili aweze kutazama habari za michero kwenye runinga na baadaye akamtembeza kwenye mitaa yote ya Tambarare. Wakati huo huo Jonathan, ambaye pia alikuwa kwenye uwanja wa michezo, alikuwa garini anaelekea nyumbani pamoja na babake Mheshimiwa Makemba.

**<u>SCENE FOUR:MAKEMBA AND SON RIDING HOME</u>**

**59. SFX: CAR BEING DRIVEN, SOUND FROM INSIDE**

**60. MHE. MAKEMBA:** Sasa, unasema kuwa... Chedede, anayeaminika kuwa mchezaji bora alifika tu uwanjani na kumvamia mwenzake na wakaanza kupigana.

**61. JONATHAN:** Ndio, lakini alikuwa na sababu ya msingi. Yule mwenzake alikuwa amemsaliti na ni sahib wake.

**62. MHE. MAKEMBA:** Hmm, kweli? Na huyu rafiki yake anaitwaje?

63. **JONATHAN:** Komora, jina lake ni Komora. Wote wawili ni watoto wa mitaani. Alafu kuna huyu msichana...

64. **MHE. MAKEMBA:** Komora. sawa... lakini, usiwe na wasiwasi,wewe ndiye utakayeipata tuzo ya mchezaji aliye na ujuzi mkubwa - M.V.P. - yaani "Most Valuable Player", na utaupata mkataba huo wa kucheza kwenye mechi za Ulaya!

65. **JONATHAN:** Ah, sina uhakika tena, baba. Baada ya kuushuhudia ujuzi wa Chedede, hata nguvu zimeniishia.

66. **MHE. MAKEMBA: (stressing)** Wewe jiamini, na mimi mzee wako, nakuunga mkono. Dereva, tafadhali ongeza sauti ya redio kidogo.

67. **SFX: MUSIC PLAYS SHORTLY.**

**68. NARRATOR:** Mhe. Makemba alikuwa anapanga kipi mara hii? Sura ya mambo inazidi kubadilika. Wakati jamii ya Makemba wakielekea nyumbani, Safina na rafiki yake mpya walikuwa wanapanda ngazi zinazoelekea nyumbani kwa shangazi Lily, bila ya kujua kinachowasubiri...

**SCENE FIVE: BACK AT AUNT LILY'S**

**69. SFX: FOOTSTEPS CLIMBING STAIRS**

**70. SAFINA: (panting)** Wee! Nimechoka ajabu. Lakini acha nikwambie ukweli, nimefurahishwa sana na kliniki ya soka ya Metogba, hapa mjini wetu. Nani angekuwa na wazo kama hilo?

**71. CHEDEDE:** Hata nami nimefurahi. Sijui kama urafiki wetu na Komora utarudi tena kama ilivyokuwa awali. Hilo linanisikitisha kwa sababu tumepitia mengi pamoja.

**72. SAFINA:** Jipe muda**.** Tumeshafika, ni hapa. Uuh! **(sigh of relief )**

**73. SFX: DOOR BEING OPENED**

**74. SHANGAZI LILY: (Very angry)** Safina! Umetoka kuzurura wapi?Nani kavunja dirisha langu? **(astonished and shocked).** Na... huyu…ni…nani.. na enh...?

**75. SFX: CRASHING AS WHEN SOMEONE FALLS**

**76. SAFINA: (Terrified)** Shangazi Lily! Una nini?...Ah, nafikiri, umekunywa sana leo. Dede, tafadhali nisaidie tumuingize ndani...

**OUTRO**

**77. NARRATOR:** Kabla ya shangazi Lily kumaliza maswali yake, alianguka na kupoteza fahamu pembeni mwa mlangoni. Kweli ilikuwa ni sababu ya pombe?Jee atakumbuka kilichotokea pombe itakapomuisha kichwani? Atafanya nini akigundua kuwa Safina alikiuka amri yake na kwenda kucheza mpira? Katika kliniki ya soka uhasama ulikuwa bayana. Nani atakayeshinda? Nani atakayeshindwa? Kwa hayo na mengine zaidi, jiunge nasi wiki ijayo katika mchezo wa "**kabumbu afrika- Ni zaidi ya mchezo!".** Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au chengine kilichotangulia tembelea kurasa zetu za tovuti www.dw world.de/lbe. Na tutafurahia maoni yako pia. Mpaka wakati mwengine... Ole! Ole! Ole! Ole!